# TANGAZO

## Kuh: MKOPO WA HAZINA KWA WATUMISHI WA UMMA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Nanyamba anawatangazia Watumishi wote kuwa amepokea mgao wa fedha Tzs **450,000,000/=** kutoka kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha kwa lengo la kuwakopesha watumishi wenye sifa za kuomba mkopo huo.

Utaratibu wa uombaji Mkopo kwa mtumishi wa Umma atatakiwa kujisajili kwenye Mtandao kupitia HAZINA PORTAL kwa kuingia katika google/Chrome ***https//als.muse.go.tz*** ndipo aweze kuomba mkopo husika.

Masharti ya Mkopo:-

i. Awe Mtumishi wa Halmashauri ya Mji Nanyamba
ii. Makato ya mshahara yasiwe 1/3 ya mshahara wake
iii. Mshahara wake lazima awe analipwa kupitia Serikali Kuu (Hazina-At Source) na awe na Cheki Namba.
iv. Awe ameajiriwa kwa masharti ya Kudumu na Pensheni
v. Mtumishi ambaye alishawahi kukopa mkopo wa Hazina kabla na ikiwa haujaisha hawezi kukopeshwa kwa sasa mpaka atakapo rejesha mkopo huo.
vi. Mkopo utarejeshwa kwa kipindi kisichozidi miezi 72 (miaka 6)
vii. Mtumishi atakatwa 3% ikiwa ni kwa ajjili ya kodi ya huduma na 1% kwa ajili ya BIMA ya mkopo ambapo vyote hukatwa wakati anaingiziwa fedha husika kwa mwombaji.
viii. **Mtumishi anayeomba mkopo huu ni lazima awe amethibitishwa kazini hivyo ajira mpya hawatakiwi kuomba mkopo huu.**
ix. **Mtumishi mwenye mashauri ya kindhamu hatakiwi kuomba mkopo huu**

CamScanner

x. Unapojisajili hakikisha unakuwa na Anwani ya barua pepe (e- mail) ambayo inatumika na unaikumbuka Nywila yake, pia uwe na Namba ya simu.

xi. Ukiwa unajisajili kwenye mfumo huu wa HAZINA PORTAL account ni lazima iwe ya mshahara unakopitia (Pamoja na taarifa nyingine zisitofautiane na za kwenye mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara E - Watumishi).

xii. **Mwisho wa kupokea maombi hay ani Tarehe 05/01/2026.**

4. Kwa watumishi wenye uhitaji na watakaoshindwa kujisajili katika anuani tajwa wafike Ofisi ya Utumishi Namba 4 kwa ajili ya maelekezo ya namna ya kujisajili na kuomba mkopo husika.

MKURUGENZI HALMASHAURI YA MJI
S. L. P 1490
NANYAMBA

Zainab S. Mgomi
**MKURUGENZI WA MJI**
**NANYAMBA**